**MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI OKTOBA, 2022 NA MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2022.**

**Dondoo za tathmini ya Oktoba, 2022 na mwelekeo wa Novemba, 2022:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2022 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan mvua pamoja na hali ya joto kwa mwezi Novemba, 2022 nchini.

a) Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2022 maeneo mengi ya nchi yaliendelea kuwa makavu. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa pwani na ziwa Victoria.
b) Katika mwezi Novemba, 2022 mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan maeneo ya Magharibi mwa nchi. Hata hivyo, mvua zinatarajiwa kuendelea kunyesha katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka (pwani ya kaskazini, kanda ya Ziwa Viktoria na Nyanda za juu kaskazini mashariki).
c) Kwa upande mwingine mvua za chini ya wastani sambamba na hali ya ongezeko la joto kiasi inatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2022.

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2022 hali ya ongezeko la joto ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ambapo kiwango cha joto la juu cha nyuzi joto 36.9°C, kilipimwa katika kituo cha Mpanda kilichopo mkoani Katavi mnamo tarehe 26 Oktoba, 2022. Halikadhalika, maeneo mengine ya nchi yaliyopima viwango vya juu vya joto zaidi ya nyuzi joto 35°C ni pamoja na kituo cha Ibadakuli nyuzi joto 35.6°C mnamo tarehe 26 Oktoba, 2022 na Tabora nyuzi joto 35.7°C tarehe 24 Oktoba, 2022. Kwa ujumla, maeneo mengi ya nchi yaliendelea kuwa makavu isipokuwa maeneo machache ya mwambao

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

wa pwani na ukanda wa Ziwa Viktoria yalipata vipindi vichache vya mvua. Kituo cha hali ya hewa kilichopo Bukoba mkoani Kagera kilipima kiwango cha mvua cha milimita 32.2 na 46.8 mnamo tarehe 2 na tarehe 29 Oktoba, 2022 mtawalia na milimita 44.9 za mvua zilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Kigoma tarehe 17 Oktoba, 2022. Aidha, vituo vingine vilivyoripoti viwango vya mvua vya juu ya milimita 10 kwa saa 24 mnamo tarehe 22 Oktoba ni pamoja na Tanga (milimita 17.1) na Pemba (milimita 14.1). Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya upepo mkali unaofikia kasi ya kilometa 40 kwa saa vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa pwani.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2022

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2022 hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani ikiashiria uwepo wa La Niña katika kipindi chote cha mwezi Novemba. Hali ya joto la bahari la chini ya wastani inatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati joto la bahari la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani.

Hali ya joto la bahari la chini kidogo ya wastani inayotarajiwa eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola sambamba na joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi inatarajiwa kusababisha msukumo hafifu wa upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi yetu ikiwa ni pamoja na maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz
**(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)**

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2022

Kwa ujumla katika mwezi Novemba 2022, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo ya magharibi mwa nchi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kwa baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambapo ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu ya Novemba, 2022. Kwa upande mwingine, hali ya ongezeko la joto kiasi inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini kutokana na upungufu wa mvua unaotarajiwa. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache katika kipindi cha Novemba, 2022. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan sehemu za miinuko sambamba na ongezeko kidogo la mvua katika wiki ya tatu ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili na ya nne ya Novemba, 2022.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, mvua za Msimu katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu na ya nne ya Novemba, 2022.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Hali ya ukavu inatarajiwa kwa ujumla. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Hata hivyo, maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Hali ya ukavu inatarajiwa kwa ujumla. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Hali ya ukavu inatarajiwa kwa ujumla. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI DISEMBA, 2022

Katika kipindi cha mwezi Disemba, 2022 mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo ya kusini mwa nchi. Hata hivyo, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 2.4 USHAURI

Upungufu wa mvua unaotarajiwa unaweza kuendelea kusababisha upungufu wa unyevunyevu katika ardhi, hivyo wakulima pamoja na jamii kwa ujumla wanashauriwa kupata na kufuata ushauri wa maafisa ugani juu ya matumizi sahihi ya mvua hizo.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Novemba, 2022 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**